# JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA FEBRUARI 2025







www.ruvuma.go.tz



# KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA FEBRUARI 2025

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## RC RUVUMA ATUNUKIWA NISHANI NNE NA MKUU WA MAJESHI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ametunukiwa nishani nne na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob John Mkunda, kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hafla hiyo imefanyika leo mkoani Ruvuma mbele ya maafisa wa jeshi na askari wa Kanda ya Kusini, ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango mkubwa wa Kanali Ahmed katika utumishi wa umma na kuimarisha usalama wa mkoa huo.

Akizungumza baada ya kupokea nishani hizo, Kanali Ahmed ameonesha furaha na kueleza kuwa ni heshima kubwa kwake kutambuliwa kwa juhudi zake. Amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuthamini kazi yake na kumpa fursa ya kuendelea kulitumikia taifa.

Aidha, amemshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi pamoja na maafisa wa JWTZ waliokuwa sehemu ya tukio hilo, akisisitiza kuwa nishani hizo ni chachu ya kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uadilifu.

Tukio hilo limeonesha mshikamano kati ya serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, huku wananchi wa Ruvuma wakilipokea kwa furaha kama ishara ya uongozi bora na maendeleo endelevu ya mkoa huo.




***Pichani katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akiwa na maafisa wengine wa waandamizi wa JWTZ wakisubiri kutunukiwa nishani na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob Mkunda katika viwanja vya JWTZ Ruhuwiko Songea***

## WAKAZI 6,000 NAMTUMBO KUPATIWA HUDUMA YA MAJI




Zaidi ya wakazi 6,000 wa vijiji vya Kilimasera, Ukiwayuyu, Mtakanini, Mterawamwahi, na Matependwe, wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma, wanatarajia kuondokana na tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kufuatia utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa visima virefu vitano.

Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imeidhinisha Shilingi milioni 300 kwa ajili ya mradi huo, ikiwa ni sehemu ya mpango wa uchimbaji wa visima 900 kwa kila jimbo nchini.

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Namtumbo, Salome Method, amesema uchimbaji wa visima hivyo ulianza Oktoba 2024 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Februari 2025.

“Kazi zilizopangwa ni uchimbaji wa visima, ujenzi wa vioski vya kuchotea maji, ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji, uwekaji wa matenki ya lita 10,000 kwa kila kijiji, ufungaji wa pampu za kusukuma maji na mifumo ya umeme wa jua,” alisema Method.

Aliongeza kuwa uchimbaji wa visima na ununuzi wa vifaa muhimu umekamilika, huku ujenzi wa vioski ukiwa umefikia zaidi ya asilimia 80.

Diwani wa Kata ya Ligera, Somebody Mhongo, ameishukuru serikali kwa kufanikisha mradi huo, hasa kwa kijiji cha Mterawamwahi ambacho kwa muda mrefu kimekuwa kikitegemea maji yasiyo safi kutoka mabonde na mito.

Mtendaji wa Kijiji cha Mterawamwahi, Joseph Haule, amesema kijiji hicho kinategemea mabomba mawili ya kupampu kwa mkono ambayo hayawezi kukidhi mahitaji ya wakazi wake.

Wakazi wa eneo hilo wameeleza kuwa tatizo la maji limeleta changamoto nyingi, ikiwemo migogoro ya ndoa kutokana na wake zao kuchelewa kurudi nyumbani wakisaka maji.

## ZIARA YA MKUU WA MAJESHI RUVUMA




Pichani wa kwanza kulia ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob John Mkunda akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed kushoto .Mkuu wa Majeshi alikuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha kumbukizi ya mashujaa wa Vita ya Majimaji wapatao 67 waliouawa kikatili na wajerumani mwaka 1906 na kuzikwa katika makaburi mawili ndani ya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Mahenge Songea

## WAJASIRIAMALI TUNDURU WAPEWA MAFUNZO



Wanavikundi vya wajasiriamali na wafanyabiashara waliokidhi vigezo vya kupata mkopo wa asilimia kumi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wamepatiwa mafunzo ya mwisho kabla ya kupokea mikopo hiyo.

Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Klasta Mlingoti, mjini Tunduru yakiwa na lengo la kuwaandaa wanufaika kwa matumizi sahihi ya mikopo ili kukuza biashara zao.

Mada zilizofundishwa zilihusisha usimamizi wa fedha, uandishi wa mipango ya biashara, mbinu mbalimbali za kibiashara, na umuhimu wa kurejesha mikopo kwa wakati.

Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika halmashauri hiyo, Bi. Jeceline Mganga, aliwasisitiza wanufaika kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili waweze kupata faida na kurejesha mikopo bila usumbufu.

“Unaporejesha kwa wakati, unajiongezea sifa ya kukopa zaidi,mikopo ii haina riba, hivyo ni fursa ya kipekee kwa wajasiriamali kuhakikisha inawanufaisha.”,alisema Jakline

Baada ya mafunzo, wanufaika walitakiwa kusaini mikataba ili kukamilisha hatua muhimu ya upatikanaji wa mikopo hiyo.

## MKUU WA MAJESHI AWATAKA WANANCHI KUWAENZI MASHUJAA



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob John Mkunda, amewataka wananchi kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuokoa Taifa dhidi ya maadui ujinga, maradhi na umasikini, pamoja na kuwaenzi mashujaa waliopigana na kufa kwa ajili ya Taifa.

Ametoa rai hiyo wakati akisoma hotuba kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya mashujaa wa Vita vya Majimaji, ambapo alikuwa mgeni rasmi wa maadhimisho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Songea

"Rai yangu ni kwamba mashujaa waliolala mahali hapa na kwingineko watutie hamasa kupambana kadri tuwezavyo ili kuokoa Taifa letu dhidi ya maadui hao, maana bado wapo. Kuendekeza uvivu, uzembe, madawa ya kulevya, rushwa, ubadhilifu wa mali za umma na malalamiko bila kufanya kazi ni kuzisaliti roho zilizoangamizwa na wakoloni kwa ajili yetu," alisema Jenerali Mkunda.

Pamoja na mambo mengine, Jenerali Mkunda amesema mashujaa hao waliangamia kuulinda utamaduni wa Mtanzania, na hivi sasa vilio ni vingi vya mmonyoko wa maadili ya kitanzania, hali inaonyesha kuwa msimamo wa mashujaa umeachwa, hivyo ni wakati wa kujitathmini na kuwaenzi mashujaa kwa

kuuenzi utamaduni uliolindwa na mashujaa kwani ndio unaotambulisha Taifa la Tanzania.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amesema maadhimisho hayo, ambayo yamekuwa yakiratibiwa na Ofisi ya Mkoa, Wizara ya Maliasili na Utalii, na Baraza la Mila na Desturi la mkoa, licha ya kuwakumbuka mashujaa, kwa mwaka huu Wizara husika imeamua kutumia maadhimisho hayo kuhamasisha utalii wa utamaduni na malikale ili kujiletea maendeleo na kutia chachu ya maadhimisho hayo.

Kanali Ahmed ameongeza kuwa, kupitia maadhimisho hayo, Mkoa umeendelea kupata fursa za kiuchumi kupitia wageni mbalimbali waliokuja kwa ajili ya maadhimisho hayo na kutembelea vivutio vilivyopo mkoani hapo.

Kwa upande wake, Chifu wa Wangoni, Emmanuel Zulu, amesema wamekuwa wakiziheshimu sana kumbukumbu hizo na zina machungu mengi kutokana na kile walichotendewa mashujaa wa Vita vya Majimaji.

Kilele cha maadhimisho ya kumbukizi ya mashujaa wa Vita vya Majimaji hufanyika Februari 27 kila mwaka, ambapo kwa mwaka huu kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni "Makumbusho ya Majimaji na Malikale Zetu kwa Maendeleo ya Utalii na Uchumi."



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akiwa na mgeni wake Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob Mkunda ndani ya viwanja vya Makumbusho ya Mashujaa wa vita ya Majimaji Songea

# RUVUMA YAFANYA TATHMINI YA MKATABA WA LIISHE




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amesema lishe duni, makuzi na udumavu madhara yake ni makubwa kama watu wote hawatawekeza nguvu kulipatia ufumbuzi.

Ameyasema hayo wakati akisoma hotuba kwenye kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe Kwa kipindi cha Julai - Desemba 2024 na programu jumuishi ya Taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kilichofanyika katika ukumbi wa Chandamali mjini Songea.

"Athari za lishe duni, makuzi, malezi pamoja na udumavu zinaweza zisionekane sasa hivi lakini madhara ni makubwa kama sote hatutoelekeza nguvu kwenye kulipatia ufumbuzi," alisema Kanali Ahmed.

Amesema kuna haja kubwa ya kujiuliza kwa nini Mkoa huu unakuwa na watu wenye udumavu na lishe duni ikiwa unazalisha chakula cha kutosha na cha ziada ambacho kinaenda kuwalisha watu wengine na kupelekea hata kufanya vibaya katika sekta ya Elimu ukilinganisha na mikoa ya jirani Mbeya, Njombe, Lindi na Mtwara.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dr. Louis Chomboko, ametaja faida za lishe bora kwa mtoto ambapo amesema anaweza kufanya vizuri katika masomo, inajenga msingi mzuri wa maendeleo, kuondoa umasikini na uchumi utapanda.

Kwa upande wake Afisa Lishe Mkoa wa Ruvuma, Joyce Kamanga, akiwasilisha tathmini ya lishe amesema hali ya lishe Mkoa wa Ruvuma udumavu kwa watoto chini ya miaka 5 asilimia 36.5, uzito pungufu kwa watoto asilimia 12.2, ukondefu kwa watoto asilimia 2.8, upungufu wa damu kwa watoto chini ya miaka 5 asilimia 30 na upungufu wa damu kwa wanawake wenye uwezo wa kuzaa asilimia 45.

Amesema Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Manispaa ya Songea na Tunduru DC wametekeleza azimio la mashine kufungwa vinu vya kuongeza virutubishi kwenye unga wa mahindi, na azimio hilo halijatekelezwa katika Halmashauri ya Songea DC, Namtumbo DC, Madaba DC, Mbinga TC na Nyasa DC.

## MACHIFU WA TANZANIA NA MALAWI WATEMBELEA MAPOSENI



Machifu kutoka ndani na nje ya Tanzania wametembelea eneo la makumbusho lililopo kata ya Maposeni, wilaya ya Songea mkoani Ruvuma , ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kilele cha kumbukizi ya mashujaa wa Vita ya MajiMaji imbacho kitafanyika , tarehe 27 Februari 2025 katika viwanja vya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji mjini Songea.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ambaye alikuwa mgeni rasmi, amewapongeza machifu kwa mshikamano wao na ushirikiano mzuri katika kudumisha mila na utamaduni.

, Amemshukuru Rais wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake katika kulinda na kuendeleza utamaduni wa Taifa.

Kanali Abbas pia amewapongeza wakazi wa Maposeni kwa kujitokeza kwa wingi na kuwasihi waendelee kushiriki kwa hamasa siku ya kilele cha kumbukizi ili kuwaenzi mashujaa 67 waliopoteza maisha yao katika vita hivyo mwaka 1906.

Amewataka waandaaji wa kumbukizi hizo kuhakikisha zinaendelea kufanyika kila mwaka ili historia hii muhimu isisahaulike kwa vizazi vijavyo.

Mgeni rasmi katika kilele cha kumbukizi ya mashujaa wa Vita ya MajiMaji anatarajiwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania




Machifu wa Mkoa wa Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na Chifu wa Wangoni Emanuel Zulu Gama Pamoja Chifu kutoka nchini Malawi wakiwa eneo la Maposeni Peramiho wilayani Songea mkoani Ruvuma ambayo ndiyo makazi ya asili ya Chifu wa wangoni

# AFISA ELIMU RUVUMA ATAJA MIKAKATI YA KUONGEZA UFAULU




Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma, Mwalimu Edith Mpinzile, ameweka bayana mikakati mbalimbali waliyopanga ili kuinua kiwango cha ufaulu katika mkoa huo.

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa elimu uliofanyika katika ukumbi wa Chandamali mjini Songea, Mwalimu Mpinzile amesema wanahitaji suala la elimu kuzungumzwa katika kila mkutano zikiwemo habari za watoro, chakula, uwajibikaji wa kila mmoja, uandikishaji, hali ya kidato cha kwanza kuripoti shuleni na ufafanuzi wa umuhimu wa Elimu.

Mikakati mingine ni kufanya mazungumzo baina ya timu itakayoundwa na walimu ambao hawatimizi wajibu wao au wanaofanya vibaya zaidi katika ufaulu wa masomo ambapo mazungumzo hayo yatashirikisha wakuu wa shule na maafisa elimu wa kata husika ili waweze kueleza sababu zinazopelekea kutofanya vizuri.

Amebainisha kuwa wamependekeza timu hiyo iundwe na Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Mwenyekiti wa Halmashauri, Maafisa Elimu wote wawili, Afisa Utumishi, Mthibiti Ubora wa Shule, na Katibu wa TSC, lengo likiwa ni kuhakikisha wadau wote wanashirikishwa katika kuboresha elimu na sio kumuachia Afisa Elimu au mtaalamu wa elimu pekee.

# RC RUVUMA ASISITIZA USIMAMIZI WA ELIMU




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewataka wadau wa elimu kuweka nguvu kwenye vipaumbele ambavyo vitamsaidia mwanafunzi kufanya vizuri kitaaluma ikiwemo usimamizi mzuri wa sekta ya elimu katika mkoa.

Ametoa rai hiyo wakati akizungumza katika mkutano wa wadau wa elimu Mkoa wa Ruvuma, uliofanyika katika ukumbi wa Chandamali mjini Songea.

Kanali Ahmed amesema wataalamu wa elimu wanazifahamu vizuri changamoto zote zinazojitokeza katika sekta ya elimu na kupelekea mkoa kufanya vibaya kitaaluma, hivyo amesisitiza usimamizi na ubunifu katika maeneo yao.

Ametoa maagizo kwa viongozi na watendaji kusimamia malengo ya ufaulu kuanzia ngazi ya kata hadi juu, kuwatambua walimu wanaofanya vizuri, shule kushiriki katika kilimo kwa lengo la kumfundisha mwanafunzi kujitegemea na kupunguza changamoto ya chakula shuleni, na wadau wote kushirikiana kuwahamasisha wazazi kuchangia chakula na watendaji wa elimu kata kusimamia uratibu mzuri wa chakula shuleni.

Naye Afisa Elimu Taaluma Mkoa wa Ruvuma, Mwalimu Frolence Ngua, amebainisha kuwa utoro wa rejareja kwa baadhi ya watahiniwa, baadhi ya walimu kutomaliza mada kwa wakati, baadhi ya wazazi kuwashawishi watoto wao kufanya

vibaya kwenye mitihani ya kitaifa, na upungufu wa walimu kwa ujumla na baadhi ya masomo ni sababu zinazosababisha ufaulu kushuka kwenye halmashauri.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Oddo Mwisho, amewataka wadau wa elimu kutambua kuwa suala la elimu ni tofauti na sekta nyingine.

## NYASA YAPITISHA BAJETI YA BILIONI 29.9



Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma imepitisha bajeti ya  shilingi bilioni 29.9 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.

Bajeti hiyo imegawanyika katika sekta mbalimbali, ikiwa ni bilioni 17.1 kwa mishahara, bilioni 4.4 kwa matumizi mengineyo, na bilioni 8.3 kwa miradi ya maendeleo na Maputo ya ndani yanatarajiwa kufikia bilioni 2.9.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Mhe. Peres Magiri, aliwasilisha salamu za Serikali na kupongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato, akibainisha kuwa yameongezeka

kutoka bilioni 1.2 mwaka 2021/2022 hadi bilioni 2.9 mwaka 2025/2026. Amewataka watumishi wa Halmashauri kuendelea na kasi hiyo ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Ametoa tahadhari juu ya tishio la mamba katika maeneo ya maji na kuwaomba wananchi kuwa waangalifu wanapovua au kuoga.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya, alisisitiza umuhimu wa wananchi kutumia vituo vya afya vilivyopo ili kuepuka kuchelewa kupata matibabu, hasa kwa wajawazito.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Starwat Nombo aliwataka madiwani kushirikiana vyema na watumishi wa Serikali katika maeneo yao kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Bw. Khalid Khalif, aliwataka madiwani kuhamasisha ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



Mbunge wa Jimbo la Nyasa mkoani Ruvuma Mhandiisi Stella Manyanya akizungumza kwenye mkutano wa Baraza la madiwani la Halmashauri ya Nyasa kwenye ukumbi wa Halmashauri hiyo Kilosa Mbambabay,mkutano huo ulifunguliwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Pers Magiri

## TANESCO INAVYOYAANGAZA MAISHA YA WANANCHI RUVUMA




Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Ruvuma limeendelea na kampeni yake ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya umeme, utunzaji wa miundombinu, na utaratibu wa kuomba huduma hiyo muhimu. Kampeni hii inatekelezwa katika maeneo mbalimbali, ikiwemo kijiji cha Mkurumusi, Kata ya Mpitimbi.

Katika ziara hiyo, wananchi walipatiwa mafunzo kuhusu njia bora za kutunza miundombinu ya umeme na kujiepusha na vitendo vya hujuma kama wizi wa mafuta ya transfoma na nyaya za umeme aina ya kopa. Aidha, walipewa maelekezo ya jinsi ya kuomba umeme kwa njia za kidigitali kwa kutumia simu janja ili kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Afisa Habari na Uhusiano wa TANESCO Ruvuma, Allan Njiro, alisisitiza kuwa kabla ya kuomba umeme, ni lazima nyumba ziwe na wiring sahihi na ziwe ndani ya maeneo yenye nguzo zinazofikika. Alieleza kuwa gharama ya kupata umeme kwa wakazi wa vijijini ni shilingi 27,000 kwa njia moja, huku gharama ya njia tatu kwa matumizi ya viwanda ikiwa shilingi 139,000, na wakazi wa mijini wakitakiwa kulipia shilingi 321,000.

## WATATU WAFARIKI DUNIA KWA KUPIGWA NA RADI NAMTUMBO



Watoto watatu wamefariki dunia na wengine wanne wamelazwa katika Kituo cha Afya Lusewa baada ya kupigwa na radi katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Mheshimiwa Ngollo Malenya, amewatembelea waathirika wa tukio hilo, akiwafariji majeruhi na kutoa mkono wa pole kwa familia za wafiwa kutoka vitongoji vya Mchangila, Ligunga, na Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa, tukio hilo limeathiri zaidi familia moja ambayo imepoteza watoto wawili, huku mtoto mmoja akitoka familia nyingine.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Mheshimiwa Malenya amewataka wananchi kuwa waangalifu nyakati za mvua, akiwahimiza kuepuka kukaa karibu na miti ili kuepuka madhara ya radi. Pia amesisitiza mshikamano wa jamii katika kusaidiana na kuwafariji waliopata msiba huo mzito.

Tukio hili linajiri wakati mvua kubwa zikiendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya nchi, na mamlaka zinahimiza tahadhari zaidi dhidi ya majanga ya asili.

## MUONEKANO WA SEKONDARI YA DKT GAMA SONGEA



Muonekano wa sekondari mpya ya Dkt Lawrence Gama iliyojengwa kwa Programu ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP) katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma

## MUONEKANO WA DARAJA LA RUHUHU WILAYANI NYASA



Muonekano wa daraja la Mto Ruhuhu linalounganisha Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma na Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe ambapo serikali ya Awamu ya Sita imetoa zaidi ya shilingi bilioni nane kutekeleza mradi huu.

# SOUWASA YAPATA MAFANIKIO MAKUBWA AWAMU YA SITA



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira SOUWASA, Mhandisi Patrick Kibasa ametangaza mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mamlaka hiyo imetekeleza miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.70, ikiongeza upatikanaji wa maji safi katika Manispaa ya Songea.

Ameitaja miradi mingine inaendelea kutekelezwa, ikiwemo Mradi wa Miji 28 unaotekelezwa katika Manispaa ya Songea wenye thamani ya takriban shilingi bilioni 145.7,

Amesema SOUWASA pia inatekeleza miradi miwili katika kata za pembezoni mwa Manispaa ya Songea. Mradi mmoja unatekelezwa katika Kata ya Subira kwa gharama ya shilingi bilioni 1.6, na mwingine katika Kata ya Lilambo na sehemu ya Kata ya Lizaboni kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5.

Serikali ya Awamu ya Sita pia imetoa zaidi ya shilingi bilioni 2 kulipa fidia kwa wananchi 975 waliopisha mradi wa maji katika Bonde la Ruhila, ambao walikuwa wakidai fidia tangu mwaka 2003.

## RC RUVUMA AWAAGIZA ,MAAFISA ELIMU KUSIMAMIA ELIMU



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewataka maafisa elimu kata wa Mkoa wa Ruvuma kujipanga upya na kutimiza wajibu wao ili kuondokana na changamoto za kutofanya vizuri kitaaluma.

Ametoa rai hiyo wakati akihitimisha mkutano wa tathmini wa maafisa elimu kata Mkoa wa Ruvuma, uliofanyika katika ukumbi wa kanisa la Anglican manispaa ya Songea.

Amewasisitiza kuwa wabunifu kutatua matatizo badala ya kulalamika, kuwasimamia walimu wafanye kazi na kutoa taarifa iwapo hawafanyi kazi ipasavyo, kuongeza kasi ya kusimamia wanafunzi kumudu stadi za KK kabla ya darasa la tatu, kuhakikisha mada zinakamilika na kupata muda wa marudio, na kuhakikisha kata zao zinafaulisha kwa asilimia zisizopungua 50 kwa daraja la kwanza hadi la tatu kwa mitihani ya kidato cha nne.

Kanali Ahmed amesema katika mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi kwa mwaka 2024 mkoa wa Ruvuma umefaulisha kwa asilimia 69.34 ambapo ufaulu umepanda kwa asilimia 0.28 kutoka ufaulu wa asilimia 69.06 kwa mwaka 2023, kwa darasa la nne ufauli ni asilimia 77 ukipanda kwa asilimia 1.76 kutoka ufaulu wa asilimia 76.01

Hata hivyo amesema kwa upande wa kidato cha pili na cha nne mwaka 2024 bado ufaulu sio mzuri, amesema ufaulu wa kidato cha pili ni asilimia 82.34 ambapo asilimia 17.66 ya wanafunzi wamebaki kidato cha pili ambao wengi huacha shule na kutofikia ndoto zao, ufaulu wa kidato cha nne ni asilimia 92.39 huku wenye daraja la kwanza hadi la tatu hawakufikia asilimia 50

Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma, Mwalimu Edith Mpinzile, amesema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya elimu.

Ameeleza kuwa, serikali inaboresha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji, kutoa fedha za uendeshaji wa shule, kulipa malimbikizo ya madeni, na kupandisha vyeo vya walimu, huku ikiendelea kusikiliza na kutatua kero za walimu na kuboresha hadhi ya walimu ili kuhakikisha Elimu inatoa matokeo bora.

## WAWEKEZAJI WAKARIBISHWA KUWEKEZA SONGEA



SERIKALI Wilayani Songea Mkoa wa Ruvuma imesema,itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya Nchi watakaohitaji kuwekeza na kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo Wilayani humo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Songea Kapenjama Ndile, baada ya kutembelea shamba la kahawa lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 3,000

linalomilikiwa na Kampuni ya Aviv Tanzania Ltd ambalo linazalisha asilimia zaidi ya tano ya kahawa inayolimwa hapa nchini.

“Kampuni ya Aviv Ltd tangu ilipoanza shughuli zake imekuwa na mchango mkubwa kiuchumi,kwa mfano mwaka jana imelipa mapato ya Sh.milioni 700 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea kutokana na mauzo ya kahawa,fedha hizi zimekwenda kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo kwa Wananchi”alisema Ndile.

Alisema kuwa,hayo ni maendeleo makubwa hivyo Serikali ya Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri zake itajenga na kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji hao ili wasikutane na vikwazo kwa kushindwa kulipa mapato na kusababisha Halmashauri kushindwa kujiendesha.

Ndile, amesifu kahawa inayozalishwa katika shamba la Aviv Ltd lililopo kijiji cha Lipokela Halmashauri ya Wilaya Songea kuwa ni tamu ikilinganishwa na kahawa inayolimwa kwenye mikoa mingine hapa nchini kutokana na radha yake.

Alisema,Wilaya ya Songea ni kimbilio kubwa kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya Tanzania wanaokwenda kuwekeza kwenye sekta ya kilimo kutokana na kuwa na mazingira rafiki ikiwemo ardhi nzuri inayofaa kwa ajili ya kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara.

Kwa mujibu wa Ndile,Wilaya ya Songea ni Wilaya Mama kwa uzalishaji wa chakula katika Mkoa wa Ruvuma na ndiyo ghala kuu la Hifadhi ya Chakula Tanzania,hivyo amewaomba wawekezaji kwenda kuwekeza kwanikuna maeneo na mazingira mazuri yanayofaa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

Dc Ndile amemtaja mwekezaji mwingine ni kampuni ya Ndolela Farm inayofanywa shughuli zake katika Halmashauri ya Madaba ambayo imepewa hekta 500 kwa ajili ya kilimo cha zao la mahindi na ngano inayotumika kama chakula na kutengeneza bia za kampuni ya Serengeti.

“siku za nyuma kulikuwa na kasumba kwa wawekezaji kuchukua malighafi za kutengeneza bia kutoka nchini Afrika Kusini wakati hapa nchini kuna malighafi za kutosha,hali hii imewarudisha nyuma wakulima wetu na wengine kukata tamaa ya kuendelea na uzalishaji wa zao hilo”alisema.

Alisema,kampuni ya Serengeti imeingia makubaliano ya kuwapa wakulima mbegu za shahiri ambao watazalisha na kuuza kwa kampuni hiyo ambapo Halmashauri ya Madaba itapata mapato na wakulima kupata watapata fedha kutokana na kilimo cha zao hilo.

## RC RUVUMA AZINDUA DAWATI LA USTAWI WA JAMII



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amezindua mradi wa uanzishwaji wa dawati la ustawi wa jamii katika stendi kuu ya mabasi ya Manispaa ya Songea iliyopo Shule ya Tanga ambapo uzinduzi huo umefanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Kanali Ahmed, amesema mkoa wa Ruvuma unakabiliwa na changamoto ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, hasa Manispaa ya Songea, hali inayosababisha kujifunza na kujiingiza katika tabia hatarishi na hata kutumwa na watu wazima kwenye matukio ya wizi, uporaji, biashara za ngono, ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.

"Katika Manispaa ya Songea kuna ongezeko la watoto wanaotumiwa katika uuzaji wa bidhaa kama vifungashio katika maeneo ya masoko, kuuza karanga, mayai na korosho, hali hii hufanya watoto wengi kuwa katika hatari ya kufanyiwa ukatili na kuhatarisha ustawi wao," alisema Kanali Ahmed.

Ameongeza kuwa uanzishwaji wa dawati la ustawi wa jamii katika stendi kuu utasaidia kuwabaini mapema watoto wanaposhuka kwenye magari, kuzuia kuingia mitaani, kubaini mahitaji na changamoto zao, na kuwapatia huduma muhimu na sehemu salama na kuwaunganisha tena na familia zao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Naye Afisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Ruvuma, Victory Nyenza, amesema kwa kushirikiana na wadau wao ambao ni Railway Children Africa wanatambulisha mradi huo ambao utatekelezwa katika stendi kuu ya mabasi ya Manispaa ya

Kw upande wake Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Hilda Ndambalilo, amesema mradi huo utaweza kuimarisha usalama wa mtoto hususani ambao wako mitaani wakifanyishwa kazi na kujumuisha wadau mbalimbali ambao watasaidia kuwaongoza watoto hao na kuhakikisha usalama wao.

## WALIMU WAASWA KUTUMIA MAFUNZO KUBORESHA ELIMU




Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mwalimu Ephraim Simbeye, amesema kuwa ili sekta ya elimu ipate matokeo yenye ufanisi, ni lazima walimu washiriki mafunzo mbalimbali ili kubadilisha mbinu za ufundishaji.

Amesema hayo wakati akikagua mafunzo ya walimu wa Sayansi na Hisabati yanayoendelea mkoani Ruvuma katika shule ya sekondari ya Wasichana ya Songea (Songea Girls) manispaa ya Songea.

Mwalimu Simbeye amewaasa washiriki kutumia maarifa wanayopata kuwasaidia walimu wengine ambao hawajapata nafasi ya kushiriki mafunzo hayo ili yalete tija na matokeo chanya kwa wanafunzi.

Amesisitiza umuhimu wa mafunzo hayo kwa walimu ambapo yatawasaidia kuboresha mbinu za ufundishaji darasani na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajifunza kwa ufanisi na kuendana na mabadiliko ya wakati.

Ameongeza kuwa sera na mtaala wa elimu wa sasa unawataka walimu kujifunza ili kuendana na mabadiliko chanya na kuhakikisha elimu ya Tanzania inaenda mbele.

## HOSPITALI YA NYASA KIMBILIO LA WATANZANIA NA MSUMBIJI




Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma iliyojengwa eneo la Nangombo imeendelea kuwa tegemeo kubwa kwa wakazi wa wilaya na nchi jirani ya Msumbiji .

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo Dr.Hussein Ngaillah anasema Hospitali hii, iliyoanza kutoa huduma rasmi mnamo Juni 2021, imeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya afya, ikihudumia kata 20 zenye jumla ya wakazi 191,193, wakiwemo wanawake 93,494 na wanaume 97,699, pamoja na vijiji vya jirani kutoka Halmashauri ya mji wa Mbinga na nchi jirani ya Msumbiji.

Kwa kipindi cha takriban miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake, Hospitali ya Nyasa imefanikiwa kutoa huduma mbalimbali muhimu kwa jamii.

Huduma hizi ni pamoja na wagonjwa wa nje (OPD), wagonjwa wa ndani (IPD), huduma za maabara, afya ya uzazi na mtoto (RCH), dawa na vifaa tiba, huduma za mionzi kama X-ray na Ultrasound, afya ya kinywa na meno, fiziotherapia, na matibabu ya dharura (EMD).

Zaidi ya hayo, hospitali inatoa huduma za afya msonge, ikiwemo matibabu ya kifua kikuu na ukoma, tohara kwa wanaume, uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi, pamoja na chanjo mbalimbali kama ile ya homa ya ini na chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi.

Tangu kuanzishwa kwake, hospitali hii imekuwa ikishuhudia ongezeko kubwa la wagonjwa wanaohudumiwa. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, hospitali ilihudumia wagonjwa 195 pekee.

Hata hivyo, idadi hii iliongezeka maradufu mwaka wa fedha 2021/2022 kufikia wagonjwa 3,325. Mwaka uliofuata wa 2022/2023 idadi iliongezeka hadi wagonjwa 6,907, na mwaka wa fedha 2023/2024 hospitali ilihudumia wagonjwa 10,374. Ongezeko hili linaonesha jinsi hospitali hii inavyoendelea kuwa tegemeo kubwa kwa jamii

Hospitali ya Wilaya ya Nyasa imekuwa ikipanuka kwa awamu tatu chini ya mfumo wa Force Account, kwa kutumia jumla ya shilingi 3,391,376,520.00 kutoka Serikali Kuu.

Awamu ya Kwanza (2018/2019): Ujenzi wa majengo saba ukiwemo jengo la utawala, jengo la wazazi, jengo la wagonjwa wa nje, huduma za mionzi, ufuaji, stoo ya dawa na maabara kwa gharama ya shilingi 1,800,000,000.00.

Awamu ya Pili (2020/2021): Ujenzi wa wodi tatu (watoto, wanawake, na wanaume) pamoja na kichomea taka kwa gharama ya shilingi 491,376,520.00.

Awamu ya Tatu (2021/2022): Ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi za upasuaji kwa wanaume na wanawake, jengo la kuhifadhi maiti, na jengo la huduma za dharura (EMD), kwa jumla ya shilingi 1,100,000,000.00 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Taifa wa UVIKO-19 (IMF).

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, hospitali hii ilipokea mradi mkubwa wa uzalishaji wa hewa tiba (Oxygen Plant), uliotekelezwa na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Afya na OR-TAMISEMI kwa gharama ya shilingi 409,000,000.00. Ufungaji wa mfumo huu ulifanywa na kampuni ya Tanzania Oxygen Gases Ltd, ukihusisha majengo ya huduma za dharura, wodi za upasuaji, na jengo la wazazi.

## RAIS SAMIA ALIVYOIFUNGUA WILAYA YA NYASA



Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma Mhe. Peres Magiri, amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara wilayani humo.

Amesema jumla ya kilomita 268 za barabara zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami, ikiwa ni pamoja na barabara ya Mbamba Bay – Kilosa, ambapo kazi bado inaendelea katika kilomita 5.5.

Hata hivyo amesema Kwa maeneo yenye miinuko mikali, kilomita 1.2 ya barabara inajengwa kwa zege, huku madaraja 12 yakiwa tayari yamejengwa.

Ameongeza kuwa barabara ya kutoka Njambe hadi Ndonga yenye urefu wa kilomita 6.9, ambayo haikuwa inafikika tangu uhuru, sasa imefunguliwa na kwamba serikali imetumia shilingi bilioni 11.2 kuboresha barabara kupitia TARURA..

Akizungumzia barabara ya lami nzito kutoka Mbinga hadi Mbambabay Mkuu wa Wilaya amesema barabara hiyo iliyogharimu shilingi bilioni 129 imeifungua wilaya ya Nyasa.

Kabla ya ujenzi wa barabara hii, wananchi walilazimika kusafiri kwa zaidi ya saa saba hadi nane, hasa wakati wa mvua, ambapo safari ilikuwa ikichukua siku nzima.

Hata hivyo, kwa sasa safari hiyo inachukua saa moja na nusu, kutoka Mbambabay hadi Mbinga hali ambayo imerahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Nyasa, Mhe. Starwat Nombo amesema barabara hizo zimekuwa mkombozi kwa wananchi kwa kuwa zimefungua milango ya fursa mbalimbali, zikiwemo za utalii katika mji wa Mbamba Bay na Mualo Bichi.

Mkazi wa Mbamba Bay, Bw. Andrea Ligola ameishukuru serikali kwa kuboresha barabara hizo, akieleza kuwa awali usafirishaji wa dagaa ulikuwa mgumu kutokana na magari kukwama na bidhaa kuharibika njiani.

Naye Emakulata Kayombo, mkazi wa Mbamba Bay, amepongeza juhudi za Rais Samia, akisema barabara hizo zimerahisisha usafirishaji wa mizigo na kuongeza idadi ya mabasi kutoka mawili hadi 12.

## RUVUMA YAFANYA TATHMINI YA ELIMU




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amesema ni ndoto ya kila Taifa kuwa na wananchi wenye elimu bora itakayowawezesha kuingia kwenye soko la ushindani wa ajira katika kila sekta.

Amesema hayo wakati akifungua mkutano wa tatu wa TAPSHA mkoa wa Ruvuma wa tathimini ya utekelezaji cha wa mtaala 2024 uliofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Songea (Songea Girls) iliyopo manispaa ya Songea.

"Ni ndoto ya kila Taifa kuwa na watu wenye afya njema, wenye elimu nzuri ambao wana fursa ya kuingia kwenye soko la ushindani wa ajira katika kila sekta, haya hayawezekani kama hatutawekeza kwa kiwango kikubwa katika elimu," alisema Kanali Ahmed.

Amesema serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, hivyo matarajio ya serikali na wazazi ni kuona matunda ya uwekezaji huo yanaleta faida chanya kwa taifa na mkoa.

Ameongeza kuwa ni wakati wa sekta zote za utendaji ndani ya mkoa kujitafakari kama zinafanya kazi inavyotakiwa, hasa sekta ya elimu kwa kuwa imekuwa ikifanya vibaya kitaifa.

Naye Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma, Mwalimu Edith Mpinzile, akitoa taarifa ya elimu ya mkoa, amesema uchambuzi walioufanya umebaini kwamba tatizo kubwa la mkoa wa Ruvuma kufanya vibaya kitaaluma ni kukosa usimamizi wa ufundishaji, hivyo iwapo kila mmoja atawajibika katika eneo lake, mkoa utaweza kufanya vizuri kitaaluma.



Baadhi ya wadau wa elimu kutoka wilaya zote Ruvuma wakiwa kwenye kikao cha tathimini ya elimu kwenye ukumbi wa Songea Girls

# MRADI BANDARI YA MBAMBABAY UTAKAVYOCHOCHEA UCHUMI



Mradi wa ujenzi wa bandari ya Mbambabay katika Ziwa Nyasa, wilayani Nyasa mkoani Ruvuma, unatarajiwa kukamilika ifikapo Januari 26, 2026, na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Mradi huu, wenye thamani ya bilioni 81, ulianza tarehe 27 Januari 2024, na unajumuisha ujenzi wa gati, majengo, na miundombinu ya zimamoto.

Mwakilishi wa kampuni inayotekeleza ujenzi, Mhandisi Timoth Mliyuka, alisema kwamba bandari hii itasaidia kuimarisha uchumi wa wilaya ya Nyasa na kuunganisha bandari ya Mtwara, ambapo mizigo itapitia kwenda nchi jirani za Zambia na Malawi. Bandari hiyo itakuwa na uwezo wa kupaki meli mbili kwa wakati mmoja.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Starwat Nombo amempongeza Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za kutekeleza mradi huo na kwamba baadhi ya bidhaa, kama mahindi, zitakuwa zikisafirishwa kwenda Malawi na Msumbiji,kupitia bandari ya Mbambabay.

Amesema mradi huo utakapokamilika, mji wa Mbambabay utafunguka, na fursa za biashara, ajira, na maendeleo zitapatikana kwa vijana na jamii kwa ujumla

## WAFANYABIASHARA WATAJENGA UCHUMI KWA KULIPA KODI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ameshiriki maadhimisho ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora Mkoani Ruvuma,

Kanali Abbas ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake katika kuhamasisha ulipaji wa kodi stahiki, na kuwashukuru wafanyabiashara kwa kujitolea katika kutoa michango ya kodi.

Katika hafla hiyo, Kanali Abbas amesema wafanyabiashara hao wameonesha uzalendo kwa Taifa na kuwaomba waendelee kuwa mabalozi wazuri kwa wengine ili waweze kujifunza kutoka kwao.

Amesisitiza umuhimu wa uhusiano mzuri kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wafanyabiashara kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi.

"Mahusiano mazuri kati ya TRA na wafanyabiashara yanajenga msingi wa ulipaji wa kodi kwa hiari na kwa wakati, jambo litakalowezesha Serikali kutimiza majukumu yake," alisema Kanali Abbas.

Aidha, amewakumbusha wafanyabiashara kutoa na kudai risiti sahihi, kwani Serikali inapata mapato kupitia risiti hizo.

Amewataka wafanyabiashara kuzingatia sheria na kujiepusha na vitendo vya ukwepaji kodi, huku akisisitiza kwamba elimu ya kodi inapaswa kuendelea kutolewa, ikizingatiwa kuwa idadi ya walipakodi inaongezeka kila siku.

Kanali Abbas ameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendelea kutatua changamoto zinazowakabili walipakodi na kutoa elimu endelevu ili kila mfanyabiashara atimize wajibu wake bila usumbufu.

## TAKUKURU RUVUMA YAFUATILIA MIRADI YA BILIONI 11



aasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo 46 yenye thamani ya jumla ya sh. Bilioni 11.025, ambapo miradi 17 yenye thamani ya sh. Bilioni 5.9 ilikutwa na mapungufu.

Changamoto zilizobainika ni pamoja na uandishi mbovu wa nyaraka (store ledger) unaosababisha upotevu wa vifaa vya ujenzi, miradi kuchelewa kuanza kutokana na mafundi wengi kutofahamu kutumia mfumo mpya wa NEST.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, alizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mahenge mjini Songea,amesema changamoto hizo ziliwasilishwa kwenye halmashauri husika ili kutafutiwa ufumbuzi, baadhi zikiratibiwa na zingine zikiendelea kufanyiwa kazi.

Ameitaja miradi yenye mapungufu ni pamoja na Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu 6 ya vyoo shule ya msingi Magingo, Ujenzi wa madarasa 6 na mabweni 2, sekondari ya Madaba, pamoja na miradi mingine ya ujenzi wa shule mpya za sekondari na mahakama ya Wilaya ya Tunduru.

Amesema TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imepokea jumla ya malalamiko 76 kutoka kwa wananchi kuanzia Oktoba hadi Disemba 2024, ambapo malalamiko 53 yaliyohusu rushwa yameshughulikiwa na uchunguzi ukiendelea. Katika kipindi hicho, TAKUKURU imefungua kesi mpya 15, na kesi 10 zimetolewa maamuzi ambapo upande wa Jamuhuri umeshinda.

## RC RUVUMA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA UJENZI VISIMA




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ameshuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambapo kwa awamu ya kwanza, halmashauri 4 za mkoa wa Ruvuma zitanufaika na mradi huo.

Akitoa taarifa katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika Kata ya Subira, Manispaa ya Songea, Mhandisi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma, Lucia Chaula, amesema mradi huo wa uchimbaji visima vya umwagiliaji utaanza na

halmashauri za Namtumbo, Madaba, Halmashauri ya Mbinga Vijijini, na Manispaa ya Songea.

Mhandisi Chaula ameeleza kuwa lengo la uchimbaji wa visima hivyo ni kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha wakulima wanaweza kuendelea kulima muda wote bila kutegemea mvua ambapo zaidi ya wakulima 540 watanufaika na visima hivyo, na zaidi ya ekari 760 zitatumia visima hivyo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kanali Ahmed amesema fedha nyingi zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya mradi huo zinatarajiwa kuzaa matunda hivyo amesisitiza kuwa kazi hiyo inapaswa kufanyika kwa kasi, uaminifu, viwango na kwa ubora uliokusudiwa.

Amebainisha kuwa miradi hiyo ya uchimbaji wa visima ambayo itagharimu zaidi ya shilingi milioni 518 katika mikoa mitatu ya Njombe, Songwe, na Ruvuma ni uwekezaji endelevu wa Serikali katika kuhakikisha inapambana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa kampuni ya M/s MNFM Construction Co, S.L.P 634 Iringa, Mubarak Ngwada, amehaidi kufanya mradi huo kwa kiwango kinachostahili, hivyo wanahitaji ushirikiano wa wenyeji wa Kata ya Subira ambapo mradi huo utatekelezwa katika manispaa ya Songea ili waweze kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Mradi huo wa ujenzi wa visima vya umwagiliaji wenye thamani ya milioni 518,728,000 unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 6 (siku 180), na mkataba huo unajumuisha mikoa mitatu ya Songwe,Njombe na Ruvuma, ambapo kisima kimoja kitahudumia ekari 40




*Muonekano wa baadhi ya majengo ya hospitali ya Halmashauri ya Madaba wilayani Songea*



JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA
Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

S.L.P 74 SONGEA

57180 RUVUMA

SIMU Nambari. 025-2602256/2602238

FAX Na. 2602144

E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz

TOVUTI: www.ruvuma.go.tz

INSTAGRAM: rs ruvuma

FACEBOOK: rs ruvuma

YOUTUBE: rs ruvuma